**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

# MWONGOZO WA NAMNA YA KUOMBA MAFUNZO YA MUDA MREFU KWA VYUO VYA VETA 2026 KUPITIA MFUMO WA MAOMBI WA VETMIS

## Hatua ya 1: Fungua Kiungo cha Maombi

Bonyeza kiungo hiki: https://vetmis.veta.go.tz/fdc

## Hatua ya 2: Anza Maombi

Ukurasa wa mwanzo (Welcome Page) utafunguka. Bonyeza **"Apply"** chini ya sehemu ya *VETA Long Courses*.

## Hatua ya 3: Ingia au Jisajili

- **Mwombaji Mpya**: Bonyeza **"Register New Account"** ili kuunda akaunti mpya.
- **Mwombaji Uliyesajiliwa**: Weka jina la mtumiaji (*Username*) na nywila (*Password*), kisha bonyeza **"Login"**.

## Hatua ya 4: Jisajili Akaunti Mpya

### 1. Taarifa Binafsi

Jaza taarifa zifuatazo:

- Jina la Kwanza (*lazima*)
- Jina la Kati (*kama lipo*)
- Jina la Mwisho (*lazima*)
- Namba ya Simu (*lazima*)
- Barua Pepe
- Mkoa
- Wilaya
- Kata
- Kijiji/Mtaa

### 2. Taarifa za Kozi

Chagua:

- Aina ya Mwombaji: **Long Course Applicant**

- Kituo cha Mafunzo
- Mwaka wa Masomo

**3. Nenosiri**

Tengeneza neno la siri kwa ajili ya akaunti yako. Ikiwa una maelezo ya ziada, yaweke. Baada ya kuhifadhi, *Username* yako itaonekana — **ihifadhi vizuri!**

## Hatua ya 5: Ingia na Kamilisha Maombi

**1. Taarifa Binafsi**

- Hakiki taarifa zako
- Weka tarehe ya kuzaliwa na jinsia

**2. Kitambulisho**

Chagua:

- Uraia
- Aina ya Kitambulisho
- Namba ya Kitambulisho
- Mahali kilipotolewa
- Tarehe ya mwisho ya matumizi ya kitambulisho
- **(Work Permit)** kama ipo

**3. Makazi**

Thibitisha taarifa zako:

- Nchi
- Mkoa
- Wilaya
- Kata
- Kijiji/Mtaa
- Mahali pa makazi
- Anwani (kama ipo)

**4. Elimu**

Chagua:

- Kiwango chako cha juu cha elimu
- Mwaka uliomaliza elimu hiyo

**5. Uchaguzi wa Kozi**

Chagua kozi kwa kupanga vipaumbele katika sekta na fani (*occupation*) hadi chaguo tatu.

**6. Taarifa za Ziada**

- Chagua ikiwa una uhitaji maalum (kama upo)
- Chagua aina ya mwanafunzi: wa **kutwa** au **bweni**
- Jaza taarifa za mlezi:
    - Majina kamili
    - Uhusiano
    - Namba ya simu
    - Barua pepe (si lazima)
    - Anwani
    - Maelezo mengine muhimu

## Hatua ya 6: Malipo

- Nenda kwenye sehemu ya **Bills and Payments**
- Bonyeza **"Request Control Number"** kupata ankara ya malipo (*Control Number*)
- Lipa kiasi cha **TZS 5,000** (kiasi hiki **hakitarudishwa**)

**Umefanikiwa!**
Subiri matokeo ya uchaguzi kupitia tovuti ya VETA au kupitia vyombo rasmi vya habari.